www.xtrapapers.com

M12/1/A1SWA/HP1/SWA/TZ0/XX

22120297

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Thursday 10 May 2012 (morning)
Jeudi 10 mai 2012 (matin)
Jueves 10 de mayo de 2012 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only.
- The maximum mark for this examination paper is *[25 marks]*.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire sur un seul des passages.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est *[25 points]*.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[25 puntos]*.


© International Baccalaureate Organization 2012

www.xtrapapers.com



*Toa maoni yako juu ya* ***moja*** *ya tungo zifwatazo.*

**1.**

MTU aliyekuwa akikanyanga ardhi ikatetemeka sasa hatazamiki-amekonda mithili ya mifupa ya panya! Uso wake umejenga peto na makunyanzi ya daima. Amepata sura ya kikongwe wa umri wa miaka tisini na…!

Kama mzee sana huyu bwana angekuwa wa umri wa miaka sitini. Nywele zake zimepoteza weusi zikaanza kuiva rangi ya hudhurungi. Wala si nywele tena; zimelainika kama zitakazo kuwa singa, ama manyoya ya paka mzee. Zimetimka mfano wa manyoya ya kuku wa kidimu aliyenyeshewa. Midomo yake imekuwa miekundu mithili ya ile ya mlevi wa *chang'aa*. Macho yamechomoa na kuyafanya kuonekana makubwa kila saa. Amekuwa si wa kulala si wa kukaa! Hana wakati maalum kwa hizo shughuli mbili. Kuna siku hushinda kutwa amelala, kuna wakati hukesha!

Mja mwenyewe amekumbana na aina zote za maradhi. Kustaafu kwake kazi kumekuwa ndio mwanzo wa balaa hiyo ya ndwele za kupishana. Akishika kuendesha tumbo, huendesha utadhani mfereji! Sikwambii kutapika – hutapika akabaki kutapika hewa. Kuitia riziki mdomoni ni kama kwamba anayaalika matapishi. Hali hii imemkosesha hamu ya kula na kumywa. Hana raha maskini wa mungu! Kuna wakati mwili wake mzima hufanya malengelenge utadhani kamwagiwa maji ya moto. Wakati huo, maji ya kuoga ni haramu kwake, maanake maradhi moto mmoja. Yakitoka haya, yaja mengine wala hayana kizuizi yajapo. Ama mwanadamu ana satua gani mbele ya kadari? Hawakusema waliosema binadamu hashi kuumbwa.

Maskini Fumbwe! Ndwele zimemtoa nyumbani akaja piga kambi hospitalini. Mafao yake ya kustaafu yote huenda kwa matibabu. Bahati yake kakumbana na daktari kijana mchangamfu, Dakta Kala Tufaha.

"Kijana mzuri sana huyu Mungu amuweke," husema Fumbwe. "Hatuna nasaba naye na muone jinsi anavyonishughulikia. Wala si mtu wa kitu kidogo."

Dakta Kala hakosi kila siku kumpitia mgonjwa wake na kumjulia hali. Awe kazini hayupo kazini atapata wasaa wa kumpitia Fumbwe. Ikitokea safiri, huwapigia wenziwe simu hapo hospitalini kujulia hali ya mgonjwa wake. Fumbwe alihisi siku zoye kwamba kulikuwa na mvuto wa aina fulani kati yao.

Dakta Kala hajawepo Pembezoni siku nyingi. Alipokuja alimkuta Fubwa na baada ya muda kaja kumchunuka. Wakawa damu zimepatana tabibu na muele wake. Hii ilikuwa mojawapo wa zile siku ambapo maradhi humpumzisha Fumbwe. Siku kama hiyo humuona amechangamka si haba! Hukaa akawatolea wagonjwa wenzake visa vya kazi alizowahi kufanya, balaa na beluwe alizokumbana nazo maishani; almradi uchangamfu moja kwa moja.

"Daktari, wewe waitwa Kala Tufaha?" Fumbwe alimuuliza Dakta Kala. Alikuwa amekaa pembeni mwa kitanda chake pale hospitalini. "Samahani kukuuliza. Imekuwaje babako aitwa Tufaha? Mimi tangu kuzaliwa najua jina Tufaha ni la kike!"

"Aah! Tufaha si jina la babangu," alisema Dakta Kala huku akimpima Fumbwe mapigo ya moyo na kuandika kitu kwenye karatasi alizokuwa nazo. "Tufaha ni mamangu."

"Mamako? Mbona hutumii jina la babako?"

"Babangu sina habari naye. Naambiwa alinitelekeza tangu nizaliwe. Nasikia yu hai lakini sijui yu wapi," alisema Kala huku macho yote kayaelekeza kwenye maandishi yake.

www.xtrapapers.com



Wakati akiyasema hayo Fumbwe alipata fursa ya kumtalii Kala. Kijana jamali. Vazi lake jeupe linampa sifa ya udaktari kweli. Mbona hiyo sura ashaiona mahali? Tabasamu ya Kala ikilandana na ya mtu ambaye akimjua ila hakumbuki ni nani. Kala, mrefu kiasi ngozi maji ya kunde. Nyewele zake kichwani kazipunguza kama za askali jeshi. Umbo lake haswa la kiaskari. Anaonekana wa kuwanda siku za baadaye.

"Baba gani atamtupa mwana mzuri kama huyu? Hakumpenda mama, mbona asimchukuwe mwanawe? Kisa cha kumtupa jongoo na mti wake," alisema Fumbwe kimoyomoyo.

"Ya baba sina habari nayo," aliendelea Kala. "Kama kusoma mamangu kajitolea mhanga kunisomesha. Alijisabilia, akajikaza kisabuni. Hivi sasa mimi hapa daktari. Natakia nini baba mimi. Kila mtu na hamsini zake eti!"

"Ushapata kukutana na babako?" Fumbwa aliuliza.

"Wala sina haja! Baki sasa nimtunze mamangu na ndugu zangu. Alhamdulillahi bibi yangu bado yu hai. Alivyonihangaikia nilipokuwa nikiinuka, naomba Insha Allah nimfurahishe vya kutosha kabla ya kusimama kwa siku yake. Akiondoka aende akiwa radhi nami."

Babu Omar, *Kala Tufaha* (2007)

www.xtrapapers.com



**2.**

**Muenzi wangu**

Muenzi wangu mkali, wafoka kikalikali,
Wawika bila kujali, kujuta kikwelikweli,
Hukujua umefeli, kalala kingalingali,
Ukatiwa pilipili, kaola kimulimuli.

Uliyonayo useme, uache kusemasema,
Bali nayo uyapime, mizani kupimapima,
Na kiu chako uzime, ni moto kuzimazima,
Mwenendo wako uhame, sishinde kuhamahama.

Shika utunzi usome, us'onwe kilimalima,
Kama hujui useme, usiwe kisemasema,
Hata kichoka uheme, upigwe kihemahema,
Uwake kama umeme, usiwe kidemadema.

Kijikwatua uimbe, usije kuvimbavimba,
Kiusahau ujumbe, usije kutambatamba,
Ukivipiga vijembe, upuzi kuambaamba,
Ukatuona vikembe, utunzi kuimbaimba.

Situone tuko chini, katula kichinichini,
Katutosa kwenye jini, kaola kibaniani,
Sisi tuko kwenye wini, kafuzu kimtihani,
Sisi hatuko ugeni, katwona kibenibeni.

Hata wafu wakuunge, si mosi kuungaunga,
Hata watu wakupinge, ni wewe kapingapinga,
Hata watu wakutenge, ni wewe katangatanga,
Hata watu wakujenge, ni wewe katingatinga.

Toka wewe ujichunge, usagwe kiungaunga,
Kinyiririka uringe, uache kumangamanga,
Ukijali ujipange, us'ende kijingajinga,
Maanguko uyatenge, uwe kijipangapanga.

www.xtrapapers.com



Siambe una ujuzi, waona kimazigazi,
Siambe una maizi, wambiwe kiwaziwazi,
Hata unapiga mbizi, miruko kipuzipuzi,
Hata unapiga tizi, mwamko kinjozinjozi.

Japo wewe ni muwinde, sianze kuwindawinda,
Sasa wewe ni mshinde, huwezi kupandapanda,
Hata wewe ni hawinde, pweke kujipindapinda,
Ila wewe ni mshonde, wanze kujilindalinda.

Samuel Mwenda, *Mashairi ya kiswahili* (2010)